

MUHTASARI WA ULIMWENGU

UPUNGUZAJI WA MADHARA UMEIMARIIKA KULIKO 2020

Kipindi cha kuanzia 2020 hadi 2022 kimeshuhudia kuongezeka kwa afua za upunguzaji wa madhara. Kwa mara ya kwanza tangu 2014, *Hali ya Upunguzaji wa Madhara Duniani (Global State of Harm Reduction)* imepata ongezeko la idadi ya nchi zinazotekeleza huduma muhimu za upunguzaji wa madhara.

Ukuaji huu umechangiwa na programu mpya za mabomba na sindano (needle and syringe programmes) (NSPs) kufunguliwa katika nchi tano za Afrika pamoja na nchi nne mpya ambazo zimeidhinisha rasmi vyumba vya matumizi ya dawa (drug consumption rooms) (DCRs)^a. Hii ni pamoja na programu moja nchini Meksiko ambayo imekuwa ikifanya kazi bila idhini rasmi tangu 2018 lakini sasa ina idhini kutoka kwa mamlaka za mitaa. Nchi tatu zimeanzisha tiba ya agonisti ya opioid (opioid agonist therapy) (OAT) kwa mara ya kwanza.

Hakuna nchi ambayo imesimamisha utekelezaji wa NSP, OAT au DCRs tangu 2020.

Mnamo 2022, tulipata:

- Nchi 92 zinazotekeleza angalau NSP moja (kutoka 86 mwaka 2020)
- Nchi 87 zilizo na angalau mpango mmoja wa OAT (kutoka 84 mnamo 2020)
- Nchi 16 zilizo na DCR za kisheria na zinazofanya kazi (kutoka 12 mnamo 2020).

Idadi ya nchi zinazotekeleza mpangilio wa naloxone kwa misingi ya kubeba nyumbani na kupitia miundo ya ugawaji-rika pia imeongezeka. Mabadiliko katika ufanuzi na mikakati ya utafiti hufanya ulinganisho wa mwaka baada ya mwaka kuwa mgumu, lakini *Hali ya Upunguzaji wa Madhara Duniani 2022* imegundua kuwa kuna nchi 35 ambapo naloxone ya kubeba nyumbani inapatikana, na nchi 21 zinazotekeleza programu za naloxone za ugawaji rika. Hata hivyo, programu hizi mara nyingi huwa

katika kiwango kidogo sana na zinaweza kuathiriwa sana na mabadiliko ya udhibiti au ufadili, hasa zile za nchi zenyekipato cha chini na cha katika kama vile Afrika Kusini, Iran na Kenya.

Hali ambayo haijashuhuduwa hapo awali, nchi 104 sasa zimeripotiwa kujumuisha marejeleo ya kuunga mkono upunguzaji wa madhara katika hati za sera za kitaifa, ikilinganishwa na 87 mwaka 2020.

Ongezeko la jumla ya kujitolea na utekelezaji wa upunguzaji wa madhara ni thibitisho ya kujitolea, uthabiti na nguvu ya jamii, mashirika ya kiraia na mashirika ya kimataifa, ambayo yametetea kwa mafanikio mtazamo wa afya na haki za binadamu wa matumizi ya dawa za kulevyta licha ya uhaba mkubwa wa rasilimali.

RASILIMALI ZISIZO SAWA, MAENDELEO YASIYO SAWA

Walakini, harakati za kupunguza madhara haziwezi kuridhika. Kiwango (coverage and scale) cha upunguzaji wa madhara bado ni kidogo, na ukosefu mkubwa wa usawa unasalia ndani na katika maeneo na nchi katika suala la ufikiaji.

Ingawa idadi kubwa ya nchi za Amerika Kaskazini, Eurasia na Ulaya Magharibi zinatекeleza NSP na OAT, programu hizi hazipo zaidi ya zilivyopo katika maeneo yote ya Afrika, Amerika ya Kusini na Karibea, na Mashariki ya Kat. Amerika Kaskazini, Mexico, Oceania na Ulaya Magharibi pekee ndizo zimeidhinisha rasmi DCRs, na hata katika nchi hizi uungwaji mkono unaweza kutoka kwa serikali ya mitaa au ya jimbo badala ya kiwango cha kitaifa.

Hata katika nchi ambapo programu za upunguzaji madhara zinatекeleza, upatikanaji, ufikiaji na ubora unasalia kuwa masuala muhimu. Huduma hasijasambazwa kwa usawa katika nyingi za nchi. Watu wanaoishi katika maeneo ya vijiji au nje ya miji mikuu, kwa mfano, mara nyingi hawahudumiwi

^a Hali ya kisheria ya DCRs inatofautiana kimataifa. *Hali ya Upunguzaji wa Madhara Duniani* hujumuisha katika kuhesabu vituo hivyo ambavyo vinaungwa mkono rasmi na mamlaka za serikali katika ngazi ya kitaifa, ndogo ya kitaifa au jiji.

vyema.

Ulimwenguni kote, watu wanaotumia dawa za kulevyaa wanaendelea kukabiliwa na kuharamishwa, unyanyapaa na ubaguzi, hali inayozua upatikanaji wa huduma. Baadhi ya watu hupitia vikwazo hivi haswa kwa ukali; hasa zaidi, wanawake, kundi la LGBTQI+, watu ambao ni wahamiaji au wakimbizi, vijana, na Weusi (Black), Wakahawia (Brown) na Watu wa kiasili (Indigenous people), ambao wote wanakabiliwa na ukosefu wa huduma zinazokidhi mahitaji yao.

Upunguzaji wa madhara katika magereza kumepanuka tu kidogo tangu 2020. Bado, ni nchi 9 pekee zinazotekeleza NSPs katika magereza: Armenia, Hispania, Kanada, Kyrgyzstan, Luxembourg, Moldova, Tajikistan, Ujeruman na Uswizi.^b Duniani, Kanada pekee ndio ina DCR yenye makao yake gerezani. Idadi ya nchi zinazotoa OAT katika magereza haijabadilika ikisalia kuwa 59. Ingawa programu za OAT sasa zinafanya kazi katika magereza ya Kosovo, Macau na Tanzania, hii inasawazishwa na data mpya inayoonyesha kwamba magereza ya Georgia, Hungary na Jordan hutoa tu OAT kwa ajili ya kuondoa dawa mwilini (detoxification).

UPUNGUZAJI WA MADHARA WAKATI WA JANGA

Tangu 2020, ulimwengu umekumbwa na majanga kadhaa makubwa ambayo yamejaribu uthabitii wa huduma za upunguzaji wa madhara. Janga la UVIKO-19 limeendelea kuwa na athari kubwa katika upunguzaji wa madhara na afya ya umma. Huduma nyingi zililazimishwa kufunga au kupunguza shughuli zake wakati hili janga lilikuwa mbaya zaidi, wakati amri za kusitisha harakati (lockdowns) na nguvu za dharura zilisababisha afya ya umma kushughulikiwa na vitengo vya usalama na jeshi, (securitisation and militarisation). Hii ilikuwa na athari kubwa kwa watu wanaotumia dawa za kulevwa.^{1,2} Hata

hivyo, huduma za upunguzaji wa madhara, hasa zile zinazoongozwa na jamii ya watu wanaotumia dawa za kulevya na jumuia ya kiraia ziliipanga ili kuhakikisha kuwa bado ziliweza kufanya kazi katika kipindi chote cha janga la UVIKO-19, kwa mfano, kwa kuongeza ufikiaji wa kuchukua nyumbani OAT na naloxone. Ni muhimu kwamba jamii ya wanaotumia dawa za kulevwa na jumuia ya kiraia - ambazo katika hali nyingi zilikuwa mstari wa mbele wa kukabiliana na UVIKO-19 - zижumuishwe katika mazungumzo ya kimataifa kuhusu maandalizi ya janga, haswa Pandemic Treaty iliopendekezwa.³

Migogoro ya kiuchumi, kisiasa, kibinadamu na mazingira pia imeweka upunguzaji wa madhara katika hatari. Nchini Afghanistan, Taliban walichukua tena udhibiti wa nchi mnamo Agosti 2021, ambayo imekuwa na athari kubwa katika utoaji wa huduma za upunguzaji wa madhara (tazama ukurasa wa XXX). Uvamizi wa Urusi nchini Ukraine mnamo Februari 2022 umesababisha uhamiaji mkubwa zaidi wa wakimbizi barani Ulaya tangu Vita vya Pili vya Dunia⁴ na kuweka huduma za upunguzaji wa madhara nchini Ukraine na nchi jirani chini ya shinikizo kubwa. Jamii na mashirika ya kiraia yameendelea kutoa huduma za upunguzaji wa madhara wakati wa mzozo huu wa kiuchumi na kibinadamu (tazama ukurasa wa XXX). Nchini Lebanon, janga la UVIKO-19 na mlipuko mkubwa katika bandari ya Beirut ulisababisha mgogoro wa kiuchumi na uhaba wa dawa muhimu za OAT mnamo 2021. Muungano wa mashirika ya kiraia za kitaifa, kikanda na kimataifa na mashirika yanayoongozwa na jamii yalifilia makubaliano na kampuni ya madawa ya Ethypharm na serikali ya Lebanon kuingiza mchango wa buprenorphine kutoka nchi za nje ili kupunguza athari za uhaba huo.⁵ Nchini Sri Lanka, migogoro ya kiuchumi na kisiasa ilisababisha uhaba wa dawa muhimu na kupunguza utendakazi wa huduma muhimu za afya, ikijumuisha upunguzaji wa madhara.⁶ Mgogoro wa hali ya hewa na hali ya hewa kali, ikiwa ni pamoja na mafuriko, moto wa nyika, ukame na mawimbi ya joto, yamesababisha majanga makubwa ya afya ya umma kote ulimwenguni ambayo yameathiri idadi

^b Mnamo 2018 na 2020, Hali ya Upunguzaji wa Madhara Ulimwenguni iliripoti kuwepo kwa NSP ya gereza huko Macedonia Kaskazini. Hata hivyo, ripoti mpya kutoka kwa mashirika ya kitaifa ya kiraia zinaonyesha kuwa NSP ya magereza haijawahi kutekelezwa ipasavyo nchini.

ya watu walio hatarini, ikiwa ni pamoja na watu wanaotumia dawa za kulevyo, watu walio gerezani na kizuizini na watu wanaokabiliwa na ukosefu wa makazi.^{7–10}

Tangu Mei 2022, ulimwengu umekabiliwa na changamoto nyingine ya afya ya umma katika mfumo wa mlipuko unaoendelea wa monkeypox. Mlipuko huo umeathiri haswa wanaume wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja na wanaume wengine wanaoshiriki ngono na wanaume. Ndani ya siku chache baada ya mkurupuko kuthibitishwa, vuguvugu la upunguzaji wa madhara na kundi la LGBTQI+ tayari zilikuwa zikishughulikia kwa ushauri kuhusu upunguzaki wa madhara na kuepuka maambukizi.^{11,12}

Jamii na mashirika ya kiraia yanayounda vuguvugu la upunguzaji wa madhara yamekabiliana na majanga haya yote kwa huruma, kujitolea na ustahimilivu. Kwa usaidizi wa serikali au bila, mashirika ya kiraia na vikundi vya usaidizi rika vimejipanga ili kuhakikisha kwamba watu wengi iwezekanavyo wanaendelea kupata huduma za kuokoa maisha na za upunguzaji wa madhara.

KUONDOA UKOLONI WA SERA YA DAWA ZA KULEVYA NA KUJENGA HARAKATI ZA UPUNGUZAJI WA MADHARA UNAOPINGA UBAGUZI WA RANGI

Katika *Hali ya upunguzaji wa madhara 2020* tuliripoti kuhusu wimbi la kutafakari kuhusu ubaguzi wa rangi na ukoloni liliofuatia mauaji ya George Floyd na afisa wa polisi huko Minneapolis, Marekani. Mabadiliko haya yameendelea kuathiri mawazo kuhusu sera ya dawa za kulevyo na upunguzaji wa madhara duniani kote.^{13–17}

Mnamo Novemba 2021, kundi la mawakili na wasomi walichapisha ripoti inayoelezea kwa kina njia ambazo sera ya dawa za kulevyo imetumiwa kuunga mkono mifumo ya mamlaka ya kikoloni na ya ubaguzi wa rangi kote ulimwenguni.¹⁵ Katika miaka ya hivi majuzi, hii imekuwa mada ya utetezi na utafiti unaofanywa

na mashirika mengi katika nchi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Afrika Kusini, Bolivia, Brazili, Indonesia na Marekani.^{13,14,18–22}

Utekelezaji wa upunguzaji wa madhara unaendelea kuathiriwa na ubaguzi wa rangi na miundo ya kikoloni. Weusi, Wakahawia na Watu wa kiasili wanaotumia dawa za kulevyo huwa na ufikajji mdogo wa huduma za upunguzaji wa madhara.¹⁵ Ubaguzi wa rangi wa moja kwa moja na wa kimuundo hufanya iwe vigumu kupata huduma kwa watu Weusi, Wakahawia na Watu wa kiasili na unasababisha Weusi, Wakahawia na Watu wa kiasili kulengwa na vyombo vya kutekeleza sheria ya dawa za kulevyo na kuzuiliwa au kufungwa bila uwiano. Hii inamaanisha kwamba mahitaji ya jamii hizi mara nyingi hayapewi kipaumbele au hupuuza.²³ Watu ambaeo ni wahamiaji au wakimbizi hukumbana na changamoto mahususi, kwa kiasi kwamba kuhama kunaweza kuwa na madhara makubwa kwa afya ya mtu.²⁴

Kuna mifano thabiti ya mashirika ya upunguzaji wa madhara yanayoongoza katika kutoa huduma kikamilifu dhidi ya ubaguzi wa rangi. Kwa mfano, shirika la *Canberra Alliance for Harm Minimisation and Advocacy in Australia* hutoa huduma za upunguzaji wa madhara zinazolenga mahususi mahitaji na desturi za jumuiya za Watu wa kiasili.²⁵

KUFIKIA JAMII AMBAZO HAZIJAHUDUMIWA VYA KUTOSHA

Harakati za kujenga vuguvugu la upunguzaji wa madhara unaopinga ubaguzi wa rangi ni mfano mmoja tu wa juhudhi zilizoandikwa katika ripoti hii kuwafikia watu ambaeo kihistoria wamekuwa hawahudumiwi vya kutosha na upunguzaji wa madhara.

Kwa mara ya kwanza, *Hali ya Kupunguza Madhara Duniani 2022* imekusanya data ya nchi baada ya nchi kuhusu utoaji wa vifaa vya uvutaji salama zaidi na matibabu ya dawa (pharmacotherapy) kwa watu wanaovuta dawa za kulevyo na kutumia vichocheo (stimulants). Utafiti wetu umegundua kuwa vifaa

vya uvutaji salama zaidi vinasambazwa katika nchi 19 duniani kote^c, na nchi 2 (Czechia na Kanada) zina programu chipukizi za matibabu ya dawa za vichochezi.

Mahitaji ya wanawake wanaotumia dawa za kulevy ya yanasalia kushughulikiwa kwa kiwango cha chini zaidi katika minge ya miktadha. Kama ilivyoripotiwa katika kila sura ya kikanda ya ripoti hii, jamii na mashirika ya kiraia wanashuhudia ya kwamba wanawake wanaotumia dawa za kulevy wanakabiliwa na vikwazo zaidi kuliko wanaume katika upunguzaji wa madhara, na kwamba kuna ukosefu wa huduma zinazolenga mahitaji ya wanawake. Wajawazito na wazazi wanakabiliwa na unyanyapaa na ubaguzi wa hali ya juu wanapopata huduma za kupunguza madhara, licha ya ushahidi wote kuonyesha ya kwamba matumizi ya dawa za kulevy na wazazi ni bora kushughulikiwa kwa upunguzaji wa madhara.^{26,27} Watu wanaojihusisha na kazi ya ngono, licha ya kupewa kipaumbele rasmi kama watu walio hatarini kupata maambukizi ya virusi nya ukimwi (key population) katika hati za sera za kimataifa, wanakabiliwa na kuhamarishwa hali ambayo huzuia ufikiaji wao na huduma za upunguzaji wa madhara.²⁸ Juhudi za mashirika ya kimataifa (global network), kama vile Women and Harm Reduction International Network na Women4GlobalFund, yamekuwa muhimu katika kuongeza ufahamu wa huu ukosefu wa usawa.

KUTOFAHILI: MGOGORO UENDELEAO WA UPUNGUZAJI WA MADHARA

Harm Reduction International imekuwa ikifuatilia uwekezaji katika upunguzaji wa madhara kwa zaidi ya muongo mmoja^d. Bado ni wafadhili wachache tu wa kimataifa wanaofadhili upunguzaji wa madhara, na uwekezaji wao unaonekana kupungua. Katika nchi za kipato cha chini na kat, ufadhili wa upunguzaji wa madhara ni 5% tu ya kiwango kinachohitajika ili kukidhi makadirio ya mahitaji ya

hudumu kwa watu wanaojidunga dawa za kulevya ifikapo 2025. Cha kusikitisha ni kwamba, pengo kati ya ufadhili unaohitajika na ufadhili ulioko limeongezeka zaidi katika miaka ya hivi majuzi.²⁹

Mnamo Septemba 2022, ujazaji wa saba wa Mfuko wa Kimataifa wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global Fund) ulifanyika. Ujazaji huo uliongeza dola bilioni 14.25, na kupungukiwa na lengo la dola bilioni 18.³⁰ Wafadhili kumi na wanane waliongeza ahadi zao kwa 30%, ikiwa ni pamoja na Umoja wa Ulaya na Ujeruman - ushahidi wa utetezi endelevu wa mashirika ya kiraia. Kulikuwa na uongozi bora kutoka kwa serikali 13 za Afrika, ambazo kwa pamoja ziliahidi zaidi ya dola milioni 50. Kwa kuzingatia ya kwamba 60% ya ufadhili wa upunguzaji wa madhara katika nchi za kipato cha chini na cha kati hutoka kwa Global Fund, ni muhimu kwamba ufadhili wa upunguzaji wa madhara ulindwe kutohana na upungufu katika ujazaji.³¹

Utafiti wa Harm Reduction International mwaka wa 2016 uligundua kuwa kufadhili kikamilifu upunguzaji wa madhara kungefikiwa kwa kuelekeza kwa upunguzaji wa madhara, 7.5% tu ya fedha zinazotumiwa kwa sheria dhidi ya dawa za kulevy.^{32,33} Miaka sita baadaye, ufadhili wa upunguzaji wa madhara bado ni mdogo sana ukilinganishwa na ule wa sheria dhidi ya dawa za kulevy. Ulimwenguni, dola bilioni 100 hutumika kwa sheria dhidi ya dawa za kulevy, na dola milioni 131 pekee zinazotumika kwa upunguzaji wa madhara.^{29,32}

Kinachotia wasiwasi hasa ni kupungua kwa uwekezaji katika utetezi wa upunguzaji wa madhara. Utetezi unaoongozwa na jamii haufadhili sana. Fursa za ufadhili wa utetezi wa upunguzaji wa madhara kuitia ruzuku za nchi nydingi kutoka Global Fund zimepungua kwa kiasi kikubwa, licha ya athari zake chanya.³⁴ Bila utetezi wa uwekezaji wa kitaifa katika upunguzaji wa madhara, huduma katika nchi za kipato cha chini na cha kati zitaendelea kutegemea ufadhili wa kimataifa ambaa unapungua.

c Hizi ni Austria, Brazil, Cheki, Estonia, Italia, Kanada, Marekani, Moldova, Slovakia, Slovenia, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uingereza, Ujeruman, Ureno na Uswizi.

d Kwa maelezo zaidi kuhusu ufadhili wa kupunguza madhara, tazama ripoti ya ufadhili ya Harm Reduction International ya 2021, *Failure to Fund: The continued crisis for harm reduction in low and middle-income countries*, inayopatikana katika <https://www.hri.global/failure-to-fund>.

Kuongezea hili, Open Society Foundation, wafadhili wakuu wa utetezi wa mageuzi ya sera za dawa za kulevwa na upunguzaji wa madhara, wamepitia mabadiliko ya kimundo na ya shirika ambayo yanaweza kuwa na athari kwa ufadhili wake katika suala hili.

Baadhi ya wafadhili wameongeza ufadhili wao kwa upunguzaji wa madhara. Hawa ni pamoja na Elton John AIDS Foundation, Robert Carr Fund na ViiV Healthcare Positive Action.^{35,36}

HAKI ZA BINADAMU NA UPUNGUZAJI WA MADHARA

Upunguzaji wa madhara ni haki ya binadamu. Inatambulika kama sehemu muhimu ya haki ya kiwango cha juu zaidi cha afya kinachoweza kufikiwa kwa watu wanaotumia dawa.³⁷ Kunyimwa ufikiaji wa upunguzaji wa madhara, ikiwa ni pamoja na katika mazingira ya kizuizini, kunakiuka marufuku ya mateso na matendo mengine ya kikatili, ya kinyama na ya kudhalilisha.^{38,39}

Katika ripoti yake ya Mei 2022 kuhusu haki za binadamu na VVU, Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu, Michelle Bachelet, alibainisha vizuizi vya ufikiaji wa upunguzaji wa madhara vinavyosabishwa na kuharamishwa, unyanyapaa na kutengwa kwa watu wanaotumia dawa za kulevya.⁴⁰ Ripoti hiyo inaangazia ukiukwaji wa haki za binadamu unaowakabili wanawake na watu walibadili jinsi wanaotumia dawa za kulevya; hasa ukatili wa kimwili na kingono, jambo ambalo huongeza uwezekano wa makundi yote mawili kuambukizwa VVU. Mada hii pia ilishughulikiwa na mashirika 18 ya haki za binadamu na upunguzaji wa madhara katika taarifa ya pamoja kwa Kikao cha

hamsini cha Baraza la Haki za Binadamu (2022), ambacho kiliangazia athari zisizo na uwiano za janga la UVIKO-19 na majibu ya serikali juu ya haki za waliotengwa na ambao wameharamishwa, ikiwa ni pamoja na watu wanaotumia dawa za kulevya, watu wanaouza ngono na kundi la LGBTQI+.⁴¹

Mnamo Juni 2022, wataalam^e wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa walitoa wito wa kukomesha kwa 'vita dhidi ya dawa za kulevya', wakisema: 'Data na uzoefu zilizokusanya na wataalamu wa Umoja wa Mataifa zimeonyesha kwamba "vita dhidi ya dawa za kulevya" vinadhoofisha afya na ustawi wa jamii na kupoteza rasilimali za umma na vita hii haitokomezi hitaji la dawa haramu na soko haramu la dawa za kulevya.' Kauli hiyo pia ilisisitiza wajibu wa mfumo wa Umoja wa Mataifa, jumuiya ya kimataifa na mataifa binafsi wanachama wa Umoja wa Mataifa kubadili uharibifu huo.⁴²

Ukiukaji wa haki za binadamu unaendelea kufanywa duniani kote kwa jina la udhibiti wa dawa za kulevya. Hizi ni pamoja na, mionganoni mwa nyingine nydingi, kunyimwa ufikiaji wa huduma za upunguzaji wa madhara, ikiwa ni pamoja na kuharamishwa kwa vifaa vya kutumia dawa za kulevya (kama vile mabomba na sindano), marufuku ya OAT (kwa mfano, nchini Urusi), na ubaguzi dhidi ya watu wanaotumia dawa za kulevya, katika utoaji wa matunzo ya VVU na homa ya ini ya virusi.⁴³

Kufikia 2021, nchi 35 ziliendelea na hukumu ya kifo kwa makosa ya dawa za kulevya. Angalau watu 131 walikuwa kwa makosa ya dawa za kulevya mwaka wa 2021. Kwa sababu ya ukosefu wa uwazi, na hata udhibiti wa habari, takwimu hii inaweza kuwa inawakilisha sehemu ndogo tu ya hukumu zote zinazohusiana na dawa za kulevya. Kulikuwa na ongezeko la 11% la hukumu za kifo zinazojulikana kwa makosa ya dawa za kulevya kutoka 2020 hadi

^e Kauli hiyo illolewa kwa pamoja na Kikundi Kazi cha Uwekaji Vizuzini Kiholela, Kikundi Kazi cha Ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana, Mwandishi Maalum wa Haki ya Afya, Mwandishi Maalum wa haki ya makazi ya kutosha, Kikundi Kazi cha Wataalamu wa Watu Wenye Asili ya Kiafrika, Mwandishi Maalum wa haki za uhuru wa kukusanyika kwa amani na kujumuika, Mwandishi Maalum juu ya athari za haki za binadamu za usimamizi na utupaji wa vitu hatarishi na taka, Mtaalamu Huru wa kufurahia haki zote za binadamu kwa wazee, Ripota Maalum wa aina za utumwa wa kisasa ikiwa ni pamoja na sababu na matokeo yake, Mwandishi Maalum wa hali ya haki za binadamu katika Jamhuri ya Kiisamu ya Iran, Mwandishi Maalum wa Usafirishaji haramu wa binadamu, hususan wanawake na watoto, Mwandishi Maalum wa mauaji ya kiholela, mauaji papohapo bila kesi iliayokamilika na ya haki au ya kiholela (the Special Rapporteur on extrajudicial, summary or arbitrary executions), na Mwandishi Maalum wa unyanasaji dhidi ya wanawake.

2021, na angalau hukumu za kifo 237 zilitolewa katika nchi 16. Takriban 10% ya hukumu zote za kifo zinazohusiana na dawa za kulevyta zilizothibitishwa mwaka wa 2021 zilitolewa kwa raia wa kigeni, hivyo basi kuibua masuala muhimu juu ya haki katika kesi na wasiwasi kuhusu haki za binadamu.⁴⁴ Licha ya maendeleo ya kukomesha hukumu ya kifo kwa makosa ya dawa za kulevyta ambayo baadhi ya nchi zimefanya (kama vile Malaysia)⁴⁵, inasalia kuwa chombo cha udhibiti wa dawa za kulevyta katika nyininge nyingi. Hakika, katika baadhi ya nchi, kuna mijadala inayoendelea ya ngazi ya kitaifa ya kurejesha au kuanzisha hukumu ya kifo kwa makosa ya dawa za kulevyta (kama vile Ufilipino na Tonga).^{44,46,47}

SIASA NA SERA

Tangu 2020, kumekuwa na maendeleo makubwa ya kisera na kisiasa katika ngazi ya kitaifa na kimataifa

ambayo yanaweza kuwa na athari kwa utekelezaji wa upunguzaji wa madhara.

Katika ngazi ya kitaifa, uchaguzi nchini Kolombia na Marekani ulishuhudia kuapishwa kwa marais ambaao wamejitolea kuunga mkono mtazamo wa kiafya wa matumizi ya dawa za kulevyta. Nchini Ufilipino, Rodrigo Duterte hakustahiki kugombea uchaguzi kwa sababu ya ukomo wa muhula mmoja wa nchi hiyo, na hivyo kumaliza urais ambaao ulikuwa umeanzisha vita dhidi ya dawa za kulevyta vilivyosababisha mauaji bila utaratibu wowote wa kisheria (extrajudicial killings) ya hadi watu 30,000.⁴⁸ Hata hivyo, ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya watu wanaotumia dawa za kulevyta na watu wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevyta unaendelea nchini humo.⁴⁹

Serikali ya Urusi imeendelea kuwa kikwazo kwa sera ya dawa za kulevyta yenye msingi wa ushahidi na inayozingatia haki katika ngazi ya kimataifa, haswa katika Tume ya Umoja wa Mataifa ya Dawa za Kulevyta (Commission on Narcotic Drugs) (CND),

KIELEZO CHA SERA YA DAWA YA KIMATAIFA (THE GLOBAL DRUG POLICY INDEX) (GDPI)

Mnamo 2021, muungano wa mashirika ya upunguzaji wa madhara ulizindua Global Drug Policy Index (GDPI).^f GDPI ndio utaratibu wa kwanza duniani wa uwajibikaji na tathmini wa kutathmini sera za kitaifa za dawa za kulevya. Lengo lake ni kukuza na kupima uwiano wa nchi na mapendekezo ya Umoja wa Mataifa kuhusu afya, haki za binadamu na maendeleo.

Fahirisi ya 2021 ilitathmini nchi 30 kote ulimwenguni. Inajumuisha viashirio 75 katika vipimo vitano: (1) kutokuwepo kwa majibu yaliyokithiri, (2) haki ya jinai na jinsi adhabu ya

mkosaji inavyoendana na uhalifu (3) upunguzaji wa madhara, (4) ufkiaji wa dawa, (5) maendeleo. Kat i ya nchi 30, Norway, New Zealand na Ureno zilipata alama za wastani za juu zaidi katika nyanja zote, huku Indonesia, Uganda na Brazil zikipata alama za chini zaidi kati ya nchi 30 zilizojumuishwa kwenye fahirisi.

Kuhusiana na upunguzaji wa madhara, Norway, Ureno na Uingereza ziliongoza nazo Brazil, Ghana na Uganda zikapata alama za chini zaidi, kati ya nchi 30.

^f Muungano huu ulijumuisha Eurasian Harm Reduction Association, the Eurasian Network of People who Use Drugs, the European Network of People who Use Drugs, the Global Drug Policy Observatory, Harm Reduction International, the International Drug Policy Consortium, the Middle East and North Africa Harm Reduction Association, the West African Drug Policy Network, the Women and Harm Reduction International Network and Youth Rise. Muungano huo ulifadhiliwa na Robert Carr Fund.

baraza la uongozi la Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Dawa za Kulevy na Uhalifu (United Nations Office on Drugs and Crime) (UNODC). Kufuatia uvamizi wa Urusi nchini Ukraine, Latvia ilipanga uteuzi wa Urusi kuwakilisha Kundi la Ulaya Mashariki katika kikundi kazi kinachohusika na kusimamia fedha na utawala wa UNODC ('FINGOV'). Balozi wa Latvia alisema: "Ninaamini kwamba mwakilishi wa nchi ambayo inatengwa zaidi na zaidi kwa sababu ya uchokozi wake dhidi ya Ukraine hatakuwa mshauri bora wa utekelezaji wa mipango ya kikanda na kimataifa." Kujibu, wajumbe wa Urusi walilazimisha kura juu ya suala hilo. Hii ilikuwa tofauti isiyo na kifani na maafikiano ya muda mrefu ambayo yamesimamia taratibu za CND na ilisababisha msuguano usio na kifani kati ya wajumbe wa nchi wanachama, ambao unaweza kuwa na athari za muda mrefu katika usimamizi wa sera ya dawa za kulevy katika CND.⁵⁰ Urusi pia imeendelea kuzuia mashirika za kiraia za upunguzaji wa madhara kupata Hali Maalum ya Ushauri (Special Consultative Status) na Baraza la Kiuchumi na Kijamii la Umoja wa Mataifa.³⁶

Kwengineko katika Umoja wa Mataifa, mwaka wa 2021, Mpango wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa kuhusu VVU na UKIMWI (UNAIDS) ulizindua *Mkakati wa Kimataifa wa UKIMWI 2021-2026: Tokomeza Ukosefu wa Usawa. Komeshwa UKIMWI.* Mkakati huu unalenga kuziba mapengo katika upatikanaji wa kinga, matibabu na matunzo ya VVU, ikivuta fikira kwa mahitaji ya watu walio hatarini kupata maambuki ya VVU (ikiwa ni pamoja na watu wanaotumia dawa za kulevy) na maeneo ambayo rasilimali na utashi wa kisiasa hautoshelezi kwa ajili

ya kukabiliana na VVU vyema.⁵¹ Zaidi ya hayo, ili kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Watu Wanaotumia Dawa za Kulevy mnamo Novemba 2021, UNAIDS ilitoa taarifa ikithibitisha dhamira yake ya kuondoa kwa sheria zinazoharamisha watu wanaotumia dawa za kulevy na ukuzaji wa huduma zinazoongozwa na jamii.⁵²


Katika Shirika la Afya Duniani (World Health Organisation) (WHO), kikao cha 2022 cha Bunge la Afya Duniani (World Health Assembly) (WHA) ilipitisha azimio la kuhakikisha Mkurugenzi Mkuu wa WHO anaendelea kutoa ripoti kwa WHA kila baada ya miaka miwili kuhusu jinsi WHO inavyoshughulikia suala la afya ya umma na matumizi ya dawa za kulevya.⁵³ WHO pia ilizindua Mikakati mipy ya *Sekta ya Afya Duniani (2022-2030)* kuhusu VVU, homa ya ini ya virusi na magonjwa ya zinaa, ambayo ni pamoja na ahadi za kupunguza madhara kwa watu wanaotumia au kujidunga dawa za kulevy na afua zilizolengwa kwa watu wanaotumia vichocheo.⁵⁴

Mnamo 2022, Global Fund pia ilizindua mkakati mipy wa 2023 hadi 2028. Hasa, mkakati huo unaiweka waziwazi Global Fund kwa ushirikishwaji na uongozi wa watu walio hatarini kupata maambuki ya VVU ili kupanua na kuboresha utoaji wa huduma.⁵⁵ Hata hivyo, watetezi juu ya Global Fund wamekosoa mkakati huo kwani haujumuishi lengo la kufadhili huduma zinazolingana na ahadi hii.⁵⁶

- 1 Asia Centre, Harm Reduction International (2021), *The Securitisation of COVID-19 Health Protocols: Policing the Vulnerable, Infringing Their Rights*.
- 2 Harm Reduction International, Larasati A, Girelli G (2021), *Caught in the Crossfire: Health and human rights impacts of COVID-19 measures on people who use drugs in Indonesia and the Philippines*.
- 3 Harm Reduction International, Burke-Shyne N (9 March, 2022), 'Letter to HC OHCHR: HRI, Community and Civil Society seek OHCHR engagement in Pandemic Treaty process' [internet]. Inayopatikana katika www.hri.global/contents/2180.
- 4 UNHCR, 'Operational Data Portal: Ukraine Refugee Situation' [internet].
- 5 Daniels C (2022), personal communication.
- 6 ACAPS (2022), *Sri Lanka: Update on the socioeconomic crisis*.
- 7 Tsagouris IE, Delcher C, Stewart SL, Gasper JJ, Shev AB, Crawford A, et al. (2022), 'The impact of California wildfires on patient access to prescription opioids', *Journal of the American Pharmacists Association*. Inayopatikana katika www.sciencedirect.com/science/article/pii/S1544319122001509.
- 8 Erens B, Williams L, Exley J, Ette I, Manacorda T, Hajat S, et al. (2021), 'Public attitudes to, and behaviours taken during, hot weather by vulnerable groups: results from a national survey in England', *BMC Public Health*, 21(1):1631.
- 9 Sarkar S (2022), 'Pakistan floods pose serious health challenges', *BMJ*, 378:o2141.
- 10 Cusack L, de Crespy C, Athanasos P (2011), 'Heatwaves and their impact on people with alcohol, drug and mental health conditions: a discussion paper on clinical practice considerations', *Journal of Advanced Nursing*, 67(4):915–22.
- 11 Gay Men's Sexual Health Alliance, (20 May, 2022), 'Monkeypox: What We Know' [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://gmsm.ca/monkeypox/>.
- 12 European Centre for Disease Prevention and Control, The Love Tank, MPACT (2022), *Navigating monkeypox: Considerations for gay and bisexual men and other men who have sex with men*.
- 13 International Drug Policy Consortium, Fordham A (26 June, 2020), 'The war on drugs is built on racism. It's time to decolonise drug policies', [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://idpc.net/blog/2020/06/the-war-on-drugs-is-built-on-racism-it-s-time-to-decolonise-drug-policies>.
- 14 Shelly S, Howell S, (2019), 'Perpetuating apartheid: South African Drug Policy', in Koram K [ed], *The War on Drugs and the Global Colour Line*. Inayopatikana katika www.jstor.org/stable/j.ctvdmwxn7.11.
- 15 Daniels C, Aluso A, Burke-Shyne N, Koram K, Rajagopal S, Robinson I, et al. (2021), 'Decolonizing drug policy', *Harm Reduction Journal*, 18(1):120.
- 16 Filter Magazine, Hoque U (3 June, 2021), 'To Decolonize Drugs, Start With Prohibition's Settler Origins' [internet, cited 21 September, 2022]. Inayopatikana katika <https://filtermag.org/decolonize-drugs-prohibition-panel/>.
- 17 Lasco G (2022), 'Decolonizing harm reduction', *Harm Reduction Journal*, 19(1):8.
- 18 Duarte EF, Freitas F da S (2019), 'Racism and drug policy: criminal control and the management of Black bodies by the Brazilian state', in Koram K [ed] *The War on Drugs and the Global Colour Line*. Inayopatikana katika www.jstor.org/stable/j.ctvdmwxn7.7.
- 19 Fransiska A (2019), 'Racism and social injustice in War on Drugs narratives in Indonesia', in Koram K [ed] *The War on Drugs and the Global Colour Line*. Inayopatikana katika www.jstor.org/stable/j.ctvdmwxn7.12.
- 20 Rede Nacional de Feministas Antiproibicionistas (2022), 'Manifesto RENFA - Nossa Partido é o Feminismo Negro Decolonial' [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://renfa.org/manifesto2022>.
- 21 Drug Policy Alliance, 'Race and the Drug War' [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://drugpolicy.org/issues/race-and-drug-war>.
- 22 Dejusticia, Drug Policy Alliance, Harm Reduction International, International Drug Policy Consortium, Release, Transnational Institute, et al. (2021) 'Descolonizar las políticas de drogas: La guerra contra las drogas y la negación de los derechos indígenas' [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://idpc.net/es/events/2021/08/descolonizar-las-politicas-de-drogas-la-guerra-contra-las-drogas-y-la-negacion-de-los-derechos-indigenas>.
- 23 Harm Reduction International, Release (2022), Submission to OHCHR on the "Promotion and protection of the human rights and fundamental freedoms of Africans and of people of African descent against excessive use of force and other human rights violations by law enforcement officersthrough transformative change foracial justice and equality", pursuant to Human Rights Council resolution 47/21.
- 24 WHO (2022), *World report on the health of refugees and migrants*.
- 25 Harm Reduction International (2021), *Integrated and Person-Centred Harm Reduction Services*.
- 26 Shirley-Beavan S, Roig A, Burke-Shyne N, Daniels C, Csak R. (202), 'Women and barriers to harm reduction services: a literature review and initial findings from a qualitative study in Barcelona, Spain', *Harm Reduction Journal*, 17(1):78.
- 27 National Advocates for Pregnant Women (2022), *Prenatal Drug and Alcohol Exposure: Science Refutes Media Hype and Enduring Myths*.
- 28 Platt L, Grenfell P, Meiksin R, Elmes J, Sherman SG, Sanders T, et al. (2018), 'Associations between sex work laws and sex workers' health: A systematic review and meta-analysis of quantitative and qualitative studies', *PLOS Medicine*, 15(12):e1002680.
- 29 Harm Reduction International, Serebryakova L, Cook C, Davies C (2021), *Failure to Fund: The continued crisis for harm reduction funding in low- and middle-income countries*.
- 30 Devex, Salldinger A, Mohammed O (22 September, 2022), Global Fund falls short of \$18B target as UK, Italy delay pledges', [internet, cited 23 September, 2022]. Inayopatikana katika www.devex.com/news/sponsored/global-fund-falls-short-of-18b-target-as-uk-italy-delay-pledges-104046.
- 31 Harm Reduction International, International Network of People who Use Drugs, Eurasian Harm Reduction Association (2022), *Key harm reduction messages for the replenishment conference, implementation of new Global Fund Strategy and NFM4*. Inayopatikana katika <https://www.hri.global/contents/2226>.
- 32 Harm Reduction International (2021), *Redirection*.
- 33 Harm Reduction International, Cook C, Phelan M, Sander G, Stone K, Murphy F. (2016), *The Case for a Harm Reduction Decade*. Inayopatikana katika https://www.hri.global/files/2016/03/10/Report_The_Case_for_a_Harm_Reduction_Decade.pdf
- 34 Harm Reduction International, Schonning S (2020), *The impact of a multi-country harm reduction advocacy grant in South-East Asia*.
- 35 Wolfe D (2022), 'Global State of Harm Reduction 2022 reviewer response'.
- 36 Bridge J (2022), 'Global State of Harm Reduction 2022 reviewer response'.
- 37 UN General Assembly, Grover A (2010), *Report of the Special Rapporteur on the right of everyone to the enjoyment of the highest attainable standard of physical and mental health*, Anand Grover, A/HRC/14/20. Inayopatikana katika <https://documents-dds-ny.un.org/doc/UNDOC/GEN/N10/477/91/PDF/N1047791.pdf?OpenElement>.
- 38 UN General Assembly, van Boven T (2003), *Report of the Special Rapporteur on Torture, and Other Cruel, Inhuman, and Degrading treatment and Punishment*, E/CN.4/2004/56. Inayopatikana katika <https://documents-dds-ny.un.org/doc/UNDOC/GEN/G03/173/27/PDF/G0317327.pdf?OpenElement>.
- 39 UN General Assembly, Nowak M (2009), *Report of the Special Rapporteur on Torture, and Other Cruel, Inhuman, and Degrading treatment and Punishment*, A/HRC/10/44. G. Inayopatikana katika <https://undocs.org/A/HRC/10/44>
- 40 Harm Reduction International (2022), *50th Session of the Human Rights Council: Drug Policy Highlights*.
- 41 Harm Reduction International et al. (2022), '50th Session of the Human Rights Council: Joint oral statement on states' responses to pandemics' [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://www.hri.global/contents/2214>.
- 42 OHCHR, United Nations Media Centre (24 June, 2022), 'End 'war on drugs' and promote policies rooted in human rights: UN experts' [internet, cited 21 September, 2022]. Inayopatikana katika <https://www.ohchr.org/en/statements/2022/06/end-war-drugs-and-promote-policies-rooted-human-rights-un-experts>.
- 43 Harm Reduction International et al. (2022), '50th Session of the Human Rights Council: joint oral statement on the right to health' [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://www.hri.global/contents/2215>.
- 44 Harm Reduction International, Girelli G, Larasati A (2022), *The Death Penalty for Drug Offences: Global Overview 2021*.
- 45 Office of the High Commissioner for Human Rights (20 June, 2022), 'Malaysia: UN experts welcome announcement to abolish mandatory death penalty', [internet, cited 22 August, 2022]. Inayopatikana katika <https://www.ohchr.org/en/press-releases/2022/06/malaysia-un-experts-welcome-announcement-abolish-mandatory-death-penalty>.
